**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
**Wizara ya Maji**
**Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga**

***Kumb. Na. CA.347/385/01/14***

**Tarehe:** 22 Juni, 2026

**TANGAZO LA FURSA ZA KUJITOLEA**

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Tanga (Tanga UWASA) ni Taasisi ya Umma inayohusika na utoaji wa huduma za maji safi na usafi wa mazingira katika Jiji la Tanga pamoja na miji ya Pangani, Muheza na Mkinga.

Kwa kuzingatia Mwongozo wa Kujitolea katika Utumishi wa Umma, Tanga UWASA inakaribisha maombi kutoka kwa wahitimu wa Kitanzania wenye sifa stahiki (hasa wanaoishi Mkoa wa Tanga) wanaotamani kujitolea ili kupata uzoefu wa kazi kwa vitendo, ujuzi wa kitaaluma na fursa ya kujifunza katika nyanja mbalimbali zinazohusiana na shughuli za Mamlaka.

## *1.0 FURSA ZA KUJITOLEA*

### 1.1 GRADUATE ENGINEER II (CIVIL/WATER RESOURCES) – 4 POSITIONS

**Kituo cha Kazi:** Tanga UWASA HQ

**Fani ya Masomo:**

Shahada ya Uhandisi wa Ujenzi, Uhandisi wa Rasilimali za Maji au sifa nyingine zinazolingana kutoka taasisi inayotambuliwa.

**Maeneo ya Kujifunza na Majukumu:**

i. Kutoa ushauri kuhusu mipango, usanifu na ujenzi wa miradi ya Mamlaka;
ii. Kushiriki katika kufanya tafiti za upembuzi yakinifu wa miradi ya maji na kuandaa mapendekezo ya miradi;
iii. Kufanya uchunguzi wa miundombinu ya maji kwa wateja wapya wanaounganishwa;
iv. Kushiriki katika utunzaji wa kumbukumbu za michoro ya usanifu;
v. Kushiriki katika usimamizi wa mikataba ya miradi;
vi. Kuandaa mipango ya usimamizi wa mazingira;
vii. Kufanya tathmini za athari za mazingira na kijamii;
viii. Kushiriki katika matengenezo ya miundombinu ya maji.

## 1.2 GRADUATE TECHNICIAN II (CIVIL/WATER RESOURCES) – 7 POSITIONS

**Vituo vya Kazi:** Tanga UWASA HQ (4), Pangani (1), Muheza (1) na Mkinga (1)

**Fani ya Masomo:**
Stashahada/FTC katika Uhandisi wa Ujenzi, Uhandisi wa Rasilimali za Maji au sifa nyingine zinazolingana kutoka taasisi inayotambuliwa.

**Maeneo ya Kujifunza na Majukumu:**

i. Kushiriki katika shughuli za mtandao wa usambazaji maji;
ii. Kusaidia katika upimaji na uchoraji ramani za miundombinu;
iii. Kusaidia ufuatiliaji wa miradi ya maji;
iv. Kushiriki katika uandaaji wa taarifa za kiufundi;
v. Kushiriki katika shughuli za kuunganisha wateja;
vi. Kutekeleza majukumu mengine ya kujifunza yatakayoelekezwa na wasimamizi.

## 1.3 VOLUNTEER ARTISAN II – 16 POSITIONS

**Vituo vya Kazi:** Tanga UWASA HQ (13), Pangani (1), Muheza (1) na Mkinga (1)

**Fani ya Masomo:**
Cheti cha Ngazi ya II/III katika Ufungaji wa Mabomba na Viungio vya Mabomba au sifa nyingine zinazolingana kutoka taasisi inayotambuliwa.

**Maeneo ya Kujifunza na Majukumu:**

i. Kusaidia ukarabati wa uvujaji wa maji;
ii. Kusaidia shughuli za kuunganisha na kukata huduma za wateja;
iii. Kushiriki katika usomaji wa dira za maji;
iv. Kusaidia matengenezo ya mifumo ya usambazaji maji;
v. Kutekeleza majukumu mengine ya kujifunza yatakayoelekezwa na wasimamizi.

## 1.4 VOLUNTEER ADMINISTRATIVE OFFICER II – 1 POSITION

**Kituo cha Kazi:** Tanga UWASA HQ

**Fani ya Masomo:**
Shahada katika Utawala wa Umma, Usimamizi wa Rasilimali Watu, Menejimenti ya Utumishi, Mipango na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Mahusiano Kazini, Biashara au Utawala wa Biashara (akiwa amebobea katika Usimamizi wa Rasilimali Watu) au sifa nyingine zinazolingana kutoka taasisi inayotambuliwa.

**Maeneo ya Kujifunza na Majukumu:**
i. Kusaidia kupanga na kusimamia mifumo ya ulinzi wa Mamlaka;
ii. Kusaidia kuhakiki mali zinazoingia na kutoka katika Mamlaka;
iii. Kusaidia na kutoa ushauri kwa menejimenti kuhusu usalama wa mali za Mamlaka;
iv. Kusaidia menejimenti katika masuala ya usalama mahali pa kazi;
v. Kusaidia usimamizi wa ofisi, jiko, majengo, usafiri na huduma nyingine;
vi. Kuhakikisha usafi wa ofisi;
vii. Kutekeleza majukumu mengine ya kujifunza yatakayoelekezwa na wasimamizi.

### 1.5 VOLUNTEER CUSTOMER SERVICE OFFICER II – 3 POSITIONS

**Kituo cha Kazi:** Tanga UWASA HQ

**Fani ya Masomo:**
Shahada katika Masoko, Sosholojia, Uhusiano wa Umma, Utawala wa Biashara au sifa nyingine zinazolingana kutoka taasisi inayotambuliwa.

**Maeneo ya Kujifunza na Majukumu:**

i. Kushiriki katika kupokea na kujibu maswali ya wateja;
ii. Kushiriki katika kushughulikia na kutatua malalamiko ya wateja;
iii. Kutekeleza majukumu yanayohusiana na bili na ufuatiliaji wa madeni;
iv. Kutunza kanzidata ya madeni na taarifa za wateja kwa mujibu wa mipango iliyoandaliwa;
v. Kufanya uchambuzi wa mara kwa mara wa madeni ya wateja;
vi. Kuwasilisha malalamiko ya wateja kwa idara/vitengo husika;
vii. Kushiriki katika kutoa taarifa zinazohitajika na wateja;
viii. Kutekeleza majukumu mengine ya kujifunza yatakayoelekezwa na wasimamizi.

## *2.0 VIGEZO VYA MWOMBAJI*

Waombaji wanapaswa:

i. Kuwa raia wa Tanzania wenye umri kati ya miaka 18 hadi 35;
ii. Kuwa na sifa zinazohusiana na nafasi anayoomba;
iii. Kuwa na vyeti halali vya taaluma kutoka taasisi zinazotambuliwa na Serikali;
iv. Kutowahi kuajiriwa katika Taasisi yoyote ya Umma baada ya kuhitimu;
v. Kuwa tayari kujitolea na kujifunza katika maeneo ya huduma ya Tanga UWASA;
vi. Kuwa na maadili mema na uadilifu;
vii. Kuwa na wadhamini wawili (2) ambao ni watumishi wa umma; na
viii. Kuwasilisha barua ya utambulisho kutoka Serikali ya Mtaa/Kijiji/Kitongoji.

## *3.0 MUDA WA KUJITOLEA*

Muda wa kujitolea utakuwa miezi kumi na miwili (12), kwa masharti ya kusainiwa kwa Mkataba wa Kujitolea na Tanga UWASA.

## *4.0 UWEZESHAJI*

Uwezeshaji utakuwa kwa mujibu wa Mwongozo wa Kujitolea katika Utumishi wa Umma na utaratibu uliowekwa na Tanga UWASA.

## *5.0MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA*

i. Kujitolea si ajira.
ii. Kushiriki katika mpango wa kujitolea hakutoi dhamana ya kuajiriwa Tanga UWASA au Taasisi nyingine yoyote ya Umma.
iii. Watakaochaguliwa watatakiwa kuzingatia sheria, kanuni, maadili ya Utumishi wa Umma na taratibu za taasisi.
iv. Waombaji watakaofaulu watasaini Mkataba wa Kujitolea kabla ya kuanza programu.

## *6.0 NAMNA YA KUTUMA MAOMBI*

Waombaji wanatakiwa kuwasilisha:

i. Barua ya maombi;
ii. Wasifu binafsi ulioboreshwa (CV);
iii. Nakala zilizothibitishwa za vyeti vya taaluma;
iv. Nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au Namba ya Utambulisho wa Taifa (NIN);
v. Barua ya utambulisho kutoka Serikali ya Mtaa/Kijiji/Kitongoji;
vi. Majina na mawasiliano ya wadhamini wawili ambao ni watumishi wa umma; na
vii. Picha mbili za pasipoti zilizopigwa hivi karibuni.

Maombi yote yaelekezwe kwa:

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mjini Tanga (Tanga UWASA),**
**S.L.P. 5011,**
**TANGA.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **05 Julai, 2026**.

Waombaji watakaochaguliwa kwenye mchujo pekee (shortlisting) wataitwa kwa ajili ya usaili.

**MKURUGENZI MTENDAJI**
**TANGA UWASA**